# HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI
# UPANGA NA MLOGANZILA

MIAKA 120
HUDUMA-ELIMU-UTAFITI
1905-2025

## UFAFANUZI KUHUSU UTARATIBU WA KUCHANGIA FIGO KWA MGONJWA ANAYEHITAJI HUDUMA HIYO

***Dar es Salaam: Septemba 2, 2025***

Hospitali ya Taifa Muhimbili ilianza kutoa huduma za ubingwa bobezi za kupandikiza figo kwa wagonjwa wenye uhitaji huo Septemba, 2017 ambapo hadi sasa jumla ya watu 106 wamenufaika na huduma hizo.

Kumekuwa na taarifa inayojirudia na kusambazwa katika mitandao ya kijamii kuhusu utaratibu wa kuchangia figo kwa wagonjwa wenye uhitaji huo. Kutokana na hilo, Uongozi wa Hospitali unapenda kutoa elimu tena juu ya utaratibu wa kutoa huduma za kupandikiza figo kama ifuatavyo;

**a.** Hospitali inatumia Kanuni za Huduma za Figo, zilizoandaliwa mwaka 2017 kwa kuzingatia miongozo na maazimio ya kimataifa na kuidhinishwa na Wizara ya Afya kabla ya kuanza huduma hizo. Ikumbukwe kuwa miongozo na maazimio ya kimataifa vinakataza biashara ya uuzaji viungo vya binadamu.

**b.** Kwa mujibu wa Kanuni hizo za Hospitali, ndugu wa karibu wa mgonjwa ndiye pekee, anayeruhusiwa kuchangia figo na uchangiaji huo hufanyika bila malipo kwa mujibu wa kanuni zetu.

**c.** Hospitali ina Kamati ya kuidhinisha mgonjwa kupandikizwa figo (Authorization Committee) ambayo inajumuisha Wanasheria, Viongozi wa Dini, Madaktari na Maafisa Ustawi wa Jamii. Kamati hiyo, hufanya vikao na kupitia maombi yote ya upandikizaji figo na kumhoji mgonjwa wa figo na ndugu yake wa damu anayetaka kumchangia figo. Pia, Kamati hii hupitia nyaraka mbalimbali za kuthibitisha uhusiano wao ikiwamo viapo, vyeti vya kuzaliwa, picha, pamoja na majibu ya vipimo vya maabara.

**d.** Hospitali inaendelea kuhakikisha kuwa upandikizaji figo unafanyika kwa mjibu wa Kanuni zake pamoja na miongozo ya kimataifa katika utoaji wa huduma hizo.

Imetolewa na;

**Aminiel Aligaesha**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma,
Hospitali ya Taifa Muhimbili.